(١)

Masomo na Mazingatio ya Kubadilisha Kibla.

Prof.Ayman AlASAR

Sifa zote njema ni zake mwenyezi Mungu Mtukufu Mola wa viumbe vyote, anayesema katika Kitabu chake Kitakatifu:

بسم الله الرحمن الرحيم

لَيْسَ الْبِرَّ أَنْ تُوَلُّوا وُجُوهَكُمْ قِبَلَ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ وَلَكِنَّ الْبِرَّ مَنْ آمَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَالْمَلَائِكَةِ وَالْكِتَابِ وَالنَّبِيِّينَ وَآتَى الْمَالَ عَلَى حُبِّهِ ذَوِي الْقُرْبَى وَالْيَتَامَى وَالْمَسَاكِينَ وَابْنَ السَّبِيلِ وَالسَّائِلِينَ وَفِي الرِّقَابِ وَأَقَامَ الصَّلَاةَ وَآتَى الزَّكَاةَ وَالْمُوفُونَ بِعَهْدِهِمْ إِذَا عَاهَدُوا وَالصَّابِرِينَ فِي الْبَأْسَاءِ وَالضَّرَّاءِ وَحِينَ الْبَأْسِ أُولَئِكَ الَّذِينَ صَدَقُوا وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُتَّقُونَ} .

Kwa maana :

{Sio wema kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa mashariki na magharibi. Bali wema ni wa anaye muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho na Malaika na Kitabu na Manabii, na anawapa mali, kwa kupenda kwake, jamaa na mayatima na masikini na wasafiri, na waombao, na katika ugombozi, na akawa anashika Sala,

na akatoa Zaka, na wanao timiza ahadi yao wanapo ahidi, na wanao vumilia katika shida na dhara na wakati wa vita; hao ndio walio sadikisha, na hao ndio wajilindao}.

Na ninashuhudia kuwa hakuna Mungu mwingine aabudiwaye kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, peke yake hana mshirika wake. Na ninashuhudia kuwa Bwana wetu na Mtume wetu Muhammad ni Mja na Mjumbe wake. Ewe Mola wetu msalie na umbariki yeye na Jamaa zake na Maswahaba wake wote.

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema zake Nyingi ambazo hazina Idadi na Rehma na Amani zimuendee Mtume Muhammad, pamoja na Familia yake na Maswahaba wake na Waislamu wote watakaofuata Mwenendo wake mpaka siku ya Mwisho Mungu atujaalie nasi tue Miongoni Mwa hao AMIN.

Na baada ya utangulizi huu.

Hakika tunu za Mola na Mazuri yake kwa Umma wa Muhammad
katika mwezi wa Shaabani ni mengi yasiyohesabika wala hayana idadi na kwamba katika matukio makubwa ambayo tunayasherehekea ndani ya mwezi wa Shaabani ni tukio la kugeuzwa kwa Kibla kutoka Nyumba ya Kudsi na kuelekea Nyumba tukufu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ya Makkah. Tukio ambalo linazingatiwa kuwa ni katika Matukio Muhimu sana katika Historia yetuvya Kiislamu, ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu aliye Mkweli, alilikubali ombi la utashi wa Kipenzi chake na Kipenzi chetu, aliyemchagua, SAW, na akamtimizia matumaini na matarajio yake ya kuelekea Kaabah Tukufu wakati wa Swala, ambacho ni Kibla cha Baba yake, Ibrahim A.S.
Mtume S.A.W, kabla ya kuhamia Madinah, alikuwa akielekea Baitul Qudsi kwa amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu wakati wa Swala zake, na aliendelea hivyo hata baada ya kuhamia Madinah kwa miezi kumi na sita au kumi na saba. Na Mtume S.A.W alikuwa akiungojea Wahyi kwa Shauku na hamu kubwa, ukimwamrisha aelekee Msikiti wa Makkah, akawa anatarajia kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa moyo wake, na akimwomba kwa ulimi wake huku akiwa na yakini ya

kujibiwa kwamba Mola Wake Mtukufu atamtimizia matumaini yake. Na Mwenyezi Mungu Mtukufu akamkubalia maombi yake hayo, na akamwamrisha aelekee Makkah wakati wa Ibada zake zote za Swala. Na katika jambo hili, anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

{قَدْ نَرَى تَقَلُّبَ وَجْهِكَ فِي السَّمَاءِ فَلَنُوَلِّيَنَّكَ قِبْلَةً تَرْضَاهَا فَوَلِّ وَجْهَكَ شَطْرَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ وَحَيْثُ مَا كُنْتُمْ فَوَلُّوا وُجُوهَكُمْ شَطْرَهُ}.

{Kwa yakini tukiona unavyo geuza geuza uso wako mbinguni. Basi tutakuelekeza kwenye Kibla ukipendacho. Basi elekeza uso wako upande wa Msikiti Mtakatifu }

Jambo ambalo halina shaka yoyote ni kwamba mtu yoyote mwenye jicho la kuzingatia na kukanyika katika Tukio la Kugeuzwa kwa Kibla atasimama katika masomo mengi na mazingatio yenye faida kutokana na ukarimu huu wa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa Mtume wake Muhammad S.A.W

Na miongoni mwa mafunzo au masomo muhimu sana ni:

Ukuu wa nafasi ya Mtume S.A.W na cheo chake cha juu pamoja na kuibainisha nafasi yake kwa Mwenyezi

Mungu Mtukufu na hili ni jambo lililoonekana wazi katika kauli yake Mtukufu alipomwambia Mtume wake S.A.W katika aya nyingi zifuatazo:

{Basi tutakuelekeza Kibla kwenye ukipendacho}.

Kutokana na fadhila zake na yeye kwa kumkirimu kwake, na kwa kuweka wazi cheo alichonacho Mtume wetu Muhammad S.A.W, kikamilifu kama alivyosema:

{Na Mola wako Mlezi atakupa mpaka uridhike}

Na kuanzia katika fadhila za mwenyezi Mungu Mtukufu kwake, na kwa nini isiwe hivyo? Wakati yeye ndiye aliyempasua kifua chake, akasema:

{Hatukukunjulia kifua chako.}

Na mwenyezi Mungu akamwondoshea mzigo wake mzito akasema:

{Na tukakuondolea mzigo wako}

Na mwenyezi Mungu akamsamehe dhambi zake akasema :

{Hakika tumekuf ungulia Ushindi wa dhaahir. Ili Mwenyezi Mungu akusamehe makosa yako yaliyo tangulia na yajayo}.

Na mwenyezi Mungu akautakasa ulimi wake na akasema:

{Wala hatamki kwa matamanio}.

Na mwenyezi Mungu akautaka moyo wake akasema:

{Moyo haukusema uwongo uliyo yaona}

Na mwenyezi Mungu:akaitakasa akili yake akasema :

{Mwenzenu huyu hakupotea, wala hakukosea}.

Na mwenyezi Mungu akayatakasa macho yake na akasema :

{Jicho halikuhangaika wala halikuruka mpaka}

Na mwenyezi Mungu akamtakasa Mwalimu wake akasema:

{Amemfundisha aliye mwingi wa nguvu}.

Na mwenyezi Mungu: akazitakasa tabia zake njema akasema :

{Na hakika wewe una tabia tukufu}.

Na mwenyezi Mungu akamtakasa yeye kwa ujumla akasema:

{Hakika nyinyi mnayo ruwaza njema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu...}

Na miongoni mwa masomo yenye faida kutokana na kugeuzwa kwa Kibla: Ni ulazima kwa Umma kushikamana na Njia au Mfumo wa Ukati Uwianifu, kwani Tukio hili kubwa limeweka Msingi wa Ukati wa Umma huu, ambapo anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

{Na vivyo hivyo tumekufanyeni muwe Umma wa wasitani, ili muwe mashahidi juu ya watu}.

Na miongoni mwa masomo na mazingatio yenye faida yanayotokana na ubadilishaji wa Kibla ni mfungamano

wenye nguvu baina ya Msikiti Mtakatifu wa Makkah na Msikiti Mtakatifu wa Akswaa iliopo Kudsi Tukufu, na kudhihirisha uhusiano wenye nguvu baina yake. Kwa hiyo Msikiti wa Makkah ndio wa kwanza kujengwa kwa ajili ya kumwabudu Mwenyezi Mungu Mtukufu hapa ardhini, na Msikiti wa Akswaa ambao ni wa pili kujengwa. Na kutoka kwa Abuu Dhari R.A amesema: Nilisema, Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu Mtukufu: Msikiti upi ambao ulijengwa mwanzo ardhini? Akasema: Msikiti wa Makkah, nikasema: Kisha Msikiti upi? Akasema: Msikiti wa Akswaa. Nikasema: Miaka mingapi ilipita baina ya Misikiti hii miwili? Akasema: Miaka arubaini, na popote itakapokukuta swala basi na uiswali kwani huo ni Msikiti.

Hakika amefungamanisha ubadilishaji wa Kibla baina ya Misikiti miwili kwa mfungamano wenye nguvu kama

alivyofungamanisha baina ya Israa na Miraji akasema Yeye Mkweli na Mtukufu:

{Ametakasika aliye mchukua mja wake usiku mmoja kutoka Msikiti Mtukufu mpaka Msikiti wa Mbali, ambao tumevibariki vilivyo uzunguka, ili tumuonyeshe baadhi ya Ishara zetu. Hakika Yeye ni Mwenye kusikia na Mwenye kuona}.

Na kwa hivyo ni wajibu kuilinda yote miwili kwa pamoja na kutoipuuzia kwani yote ni amana kwa Waislamu wote mpaka Mwenyezi Mungu Mtukufu atakapoyamaliza Maisha ya Ulimwengu huu na vilivyomo ndani yake.

Na tunapolizingatia tukio la kubadilishwa kwa Kibla, hakika sisi tutaliona jambo la ndani mno na linahitaji tusimame katika sababu na hali za mabadiliko na mageuzi ya zama zetu. Ambapo mabadiliko ya kweli sio katika wakati na sehemu, bali ni katika kuelewa maana

ya mabadiliko hayo na kasi ya kutekeleza amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa hiyo basi, zingatio sio katika kuelekea Upande wa Mashariki na Magharibi bali ni katika kuelekea kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na ukweli wa kumtegemea yeye , na mabadiliko ya kweli ya kujiepusha na uharibifu na ufisadi kuelekea katika ujenzi na marekebisho, na kutoka katika ukosefu wa ajira na uzembe kuelekea katika kazi zaidi na uzalishaji, na kutoka katika umwagaji damu na kuelekea katika kuyalinda maisha ya watu, na kutoka katika ukiukwaji wa heshima za watu au kushambulia mali za Watu na heshima zao kuelekea katika kuzilinda ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema katika aya yafuatayo:

{Sio wema kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa mashariki na magharibi. Bali wema ni wa anaye muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho na Malaika na

Kitabu na Manabii, na anawapa mali, kwa kupenda kwake, jamaa na mayatima na masikini na wasafiri, na waombao, na katika ugombozi, na akawa anashika Sala, na akatoa Zaka, na wanao timiza ahadi yao wanapo ahidi, na wanao vumilia katika shida na dhara na wakati wa vita; hao ndio walio sadikisha, na hao ndio wajilindao}.

Maana ya hayo yote ukifanya kitu chochote lazima ufanye hivyo kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu,bila ya riyaa au masilahi ya binafsi ili Mwenyezi Mungu Akubarikie maisha yako na familia yako dunia na akhera.

Na ninaisema kauli yangu hii, na ninamwomba msamaha Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ajili yenu na kwa ajili yangu.

* * *

Alhamdu lillahi rabi Alalameen wa assalatu wa alsalamu ala sayyedna Muhammad (s.a.w).

Katika hutoba ya pili tunazungumzia juu ya umuhimu wa uchanya na msimamo thabiti wa kila mtu.

Ndugu zangu Waislamu.

Sifa zote njema ni zake mwenyezi Mungu Mtukufu Mlezi wa viumbe vyote. Na ninashuhudia kuwa hakuna Mungu mwingine isipokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, peke yake asiye na mshirika, na ninashuhudia kuwa bwana wetu na Mtume wetu Muhammad ni Mja na Mjumbe wake. Ewe Mola wetu mswalie na umpe rehma Mtume wetu na umbariki, yeye, na Jamaa zake, na Maswahaba wake wote, na atakayewafuata kwa Wema mpaka siku ya Malipo.

Ndugu zangu Waislamu.

Hakika Maisha ya Mtume (S.A.W) yaliweza kupambanulika kwa uzuri katika nyakati zote za Maisha hayo, Mtume S.A.W alishuhudia akiwa na umri wa miaka kumi na tano, Makubaliano ya Fudhuul

yaliyoitishwa na makabila ya Kikureshi na wakakusanyika katika nyumba ya Abdullahi bin Jud-aan, wakawekeana mkataba na kukubaliana kwamba wasimkute mtu yoyote aliyedhulumiwa Makkah katika Watu wake au wageni wake isipokuwa watamnusuri na waliungana pamoja dhidi ya aliyedhulumu wakiwa pamoja na aliyedhulumiwa mpaka wakamrejeshea haki yake. Akasema Mtume(S.A.W): Hakika mimi nilishuhudia nyumbani kwa Abdillahi bin Jud-aan makubaliano ambayo niliyapenda, na hata kama ningeliitwa kwa ajili yake Katika Uislamu basi ningeuitikia wito wake.

Na katika umri wa miaka thelathini na tano, Mtume S.A.W alishiriki katika ukarabati wa Kaabah kwa kubeba mawe begani mwake na akaondosha mianya ya tofauti iliyotaka kujitokeza baina ya koo za Kikureshi zama hizo, ambapo walizozana mzozo mkubwa baina yao juu ya

utashi wa kila mmoja wao apate utukufu wa kulibeba Jiwe jeusi na kuliweka katika sehemu yake, na wote wakaafikiana na rai ya Mtume S.A.W ambapo kila ukoo uliwakilishwa katika kuliweka Jiwe hilo katika sehemu yake. Kisha baada ya kupewa Utumue, Mtume akaja kuwa Ruwaza njema katika uchanya, kama ambavyo alikuwa ni Ruwaza na mfano mwema wa Kiongozi katika kila kitu, na akawa Mtume S.A.W Mtu Bora katika Watu, na akawa muhimizaji bora, na mkarimu aliye zaidi katika Watu. Na kutoka kwa Ali R.A amesema: Tulikuwa sisi pindi ukali wa mapigano unapofika kileleni na watu wakakutana na wengine, tulimlinda Mtume S.A.W na hawi yoyote katika sisi karibu na adui kuliko Mtume S.A.W.Na hakika Mtume S.A.W alishirikiana na Maswahaba wake katika uchimbaji wa Handaki. Mtume S.A.W ameuasa Umma wake uwe na uchanya na akauonya na uhasi aliposema: Mtu hapaswi kuwa

mfuasi wa asichokijua, akasema: Mimi niko pamoja na watu wakifanya vyema na mimi nitafanya vyema na wakifanya vibaya na mimi nitafanya vibaya, lakini ziwekeni pazuri nafsi zenu kwa namna ambayo, watu wanapofanya vizuri na nyinyi mnafanya vizuri, na watakapokosea na kufanya vibaya basi nyinyi msiwadhulumu Watu .

Na uchanya maana yake ni mtu kujihisi kuwa ana majukumu katika Dini yake na nchi yake, kwani mapenzi ya mtu kwa nchi yake hayawi katika hisia zake, silika na anavyojisikia tu bali lazima utafsiriwe kwa mwenendo wa mtu na Utendaji wake.

Kwa hiyo Mtu Chanya: ni yule anayeendana na masuala ya kijamii na anaathirika na mazingira yake na anayaathiri kwa kila jambo lenye manufaa. Hapana shaka yoyote kwamba miongoni mwa mionekano ya Uchanya ni kushiriki kweli kweli katika kila

kinachoitumikia jamii hiyo, na kupelekea Ujenzi wa Nchi na kuulinda Usalama na utulivu wa Nchi hizo. Iwe ni kwa kuzilinda au kwa kufanya kazi vizuri na kwa kuitekeleza ipasavyo au kwa kuleana na kuhurumiana baina ya wananchi wa Nchi moja au hata kwa ushiriki wa kweli ulio Chanya katika haki zote za Kikatiba na Kitaifa pamoja na kujipamba na kiwango cha juu cha viwango vya Uaminifu kwa kutoa kila kitu ambacho kinaweza kuliinua Taifa kwa mujibu wa yatokanayo na moyo wa Uzalendo ulio huru kwa kila mzalendo mwenye sifa njema. Ambapo anasema Mshairi wa Misri Ahmad Shauqiy:

وَلِلأَوطانِ في دَمِ كُلِّ حُرٍّ يَدٌ سَلَفَت وَدَينٌ مُستَحِقُّ

Kwa maana:

Na Mataifa yanaimarika kwa Damu ya kila aliye huru Mkono umeupa na Deni lina haki ya kulipwa

Ewe Mola wetu tuoneshe Haki ya kweli na utujaalie tuwe ni wenye kufuata, na utuoneshe batili ya kweli na uturuzuku njia ya kuiacha, na uzilinde nchi zetu na wakazi wake na majeshi yake na askari wa usalama wake.

Kwa hiyo, kongole kwa mtu aliyemsamehe mwenzake aliyemdhulumu na akamuunga undugu yule aliyemkata undugu huo, na akamfanyia wema yule aliyemfanyia uovu.

Ewe Mola wangu zipe nafsi zetu uchamungu wake, na uzitakase kwani Wewe ni mbora wa kutakasa nafsi, na Wewe ndiye kiongozi wa nafsi zetu na Mola wake.Na dua yetu ya mwisho ni Alhamdulillahi Rabi Alalameen Wassalamu Alaykum warahmatullahi wabarakatuh.